Liitie Jina La Bwana

(Call On The Name Of The Lord)

Na

J. D. Logan

Liitie Jina La Bwana

(Call On The Name Of The Lord)

Na

J. D. Logan

Novemba 5, 2011

Liitie Jina La Bwana

Mdo. 2:21, "*Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.*"

Mengi yamesemwa kuhusu kifungu hiki na maoni mengi yametolewa. Wengi na zaidi hupotosha maandiko, wakidhani ndiyo wenye ukweli. Hataivyo wengi hujiegesha katika wazo moja: kwamba hii inamanisha tu kuita kwa sauti kubwa jina la Yesuhakuna kinachoweza kuwa mbali na ukweli.

Kuita katika mazingira haya inamanisha *kuomba* kwa jina la Bwana. *Kuomba* inamanisha "kumwita Mungu kwa ajili ya baraka, msaada, uvuvio, kusaidiwa, n.k." Mara nyingi, mengi hujumuika hapa kuliko kulia kwa sauti jina la Yesu.

Mfumo kama huo unahusika tunapo "ita jina la sheria (jamii)." Kama *tukiomba* sheria, tunafanya hivyo kwa *kuendana* na sheria. Hakuna hata mmoja katika akili yake timamu anaweza *kuomba* jina la sheria pasipo *kuendana* na kanuni ya kisheria.

Kwa mara ya kwanza wanadamu walipoanza, "Kuliitia Jina La Bwana" ni pale Enoshi alipozaliwa, mwana wa Sethi, mjukuu wa Adamu, tunaambiwa, "*…hapo ndipo watu walipoanza kuliitia jina la BWANA.*" (Mwa. 4:26).

Neno la Kiebrania lililo tumika hapa ni qara na inatafsiriwa kama, "lilia, hubiri, matanga (zo), julisha, julisha". Maana yake iko wazi: watu walianza kuomba Bwana, na kulitangaza jina lake mbali.

Matumizi mengine ya msemo huu ipo katika Zab. 105:1, "*…liitieni jina lake, wajulisheni watu matendo yake…*". Isa. 12:4, "*Mshukuruni BWANA, liitieni jina lake; yatangazeni matendo yake kati ya mataifa…*". Pia, angalia Yoeli 2:32; Zefania 3:9.

Hii inaturudisha katika kifungu chetu na kutuongoza katika kile ambacho kinafuata kimaantiki: matokeo ni yapi ya *kuliitia jinaa la Bwana*?

Katika Rum. 10:13, tunaambiwa, Wayahudi au Mataifa, "*Kwa kuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokoka.*"

Katika 1 Kor. 1:2, tunasoma, "*…kwa kanisa la Mungu, …wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, (fanya takatifu, takasa, weka wakfu), walioitwa wawe watakatifu, (Wakristo, watakatifu), pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali…*".

Kwa vile *kuliitia jina la Bwana* huleta wokovu na kuingia ndani katika mwili wa Kristo huleta wokovu na kuingia katika mwili wa Kristo, inafuatia kwamba chochote ambacho maandiko hufunua kuwa muhimu kwa wokovu uanzisha *kuliitia jina la Bwana.*

Vitu Ambavyo Tunaokolewa Kwalo – Upande wa Mungu

- Yohana 3:17, "*…Mungu alimtuma (Kristo) ulimwenguni…baali ulimwengu uokolewe katika yeye.*"
- Tito 3:5, "*…bali kwa rehema yake (Mungu) alituokoa…*".
- Mdo. 15:11, "*Bali twaamini kwamba tutaokoka kwa neema ya Bwana Yesu…*".
- Mdo. 4:12, *"…kwa maana hapana jinaa jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"
- Rum. 5:10, "*…zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake.*"

Mungu amemtengezea mwanadamu ili apate wokovu. Hii ni sehemu ya mpango wake. Mwanadamu haakuistaahili; au mwanadamu haakuilipia kwa kazi yo yote waliyofanya. Paulo anaelezea sehemu ya Mung katika mpango wa wokovu vizuri sana katika Efe. 2: 8-9, "*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu.*"

Vitu Ambavyo Tunaokolewa Kwalo – Sehem ya Mwadamu

Yesu, tazamio la rehema ya Mungu, toka mwanzo, alifundisha kwamba mwanadamu anaapaswa kuendana na vipengele vya rehema ya Mungu, injili. Yohana 14:15, "*Mkinipenda, mtazishika amri zangu.*" Hakuna mtu awezaye kuisema vyema. Ni kwa kutii kwetu maagizo ya Kristo na mitume wake kwamba tunaonyesha upendo wetu kwake.

Hii, basi, ni sehemu ya mwanadamu katika mpango wa Mungu wa wokovu.

Imani.

- Rum. 10:9, "*Kwa sababu <u>ukimkiri</u> Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na <u>kuamini</u> moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, <u>utaokoka</u>.*"

- Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Toba.

- Mat. 9:13, "*…kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.*"
- 2 Pet. 3:9, "*…(Mungu) maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.*"

Kukiri.

- Luka 12:8, "*Nami naawambia, kila atakayenikiri mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri yeye mbele ya malaika wa Mungu.*"
- Rum. 10:10, "*…kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

Ubatizo.

- 1 Pet. 3:21, "*Mfano wa mambo hayo ni ubatizo unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.*"
- Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka;…*".

Kwa ufupi

Zote hizi ni, kama waandishi wa injili walivyosema, vitu ambavyo tunaokolewa kwalo. sipendekezi kwamba huu ndiyo wajibu wote wa mwanadamu: hakika ni mwanzo tu "kanuni za kwanza", (Ebr. 6:1).

Wokovu ni hali ya utimilifu, kama tunavyosoma katika Ufu. 2:26, "*Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa,*".

Siyo tendo moja la utii lenyewe litaleta wokovu lakini pia katika kuungana na matendo yote ya utii.

HIVYO BASI, TUNAHITIMISHA KWAMBA, "*KULIITIA JINA LA BWANA*" INAWEZA KUPATIKANA TU KWA KUFUATA NA KUTII AMRI ZOTE ZA BWANA WETU NA MITUME WAKE.

Katika kuupenda kweli,

Ndg yenu katika Kristo,

J D Logan